Ushirika

Na

F.H. Stringham

(The Communion)

Mwanzo kabisa napenda kutambua, mchango wa ndugu W. C. Stephens, Vancouver, Washington; N. E. Kellems, Temple City, California, na C. M. Brockman, Chico, California. Katika kutengeneza kutabu hiki.

Imeandaliwa

Na

Ellis P. Forsman

Nukuu zote za vifungu vya Biblia viko katika toleo la Kiswahili

Ushirika

Au

Meza ya Bwana

"*Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mung…*" (1 Pet. 4:11). "*Wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli. Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa kama kikipokewa kwa shukrani.*" (2 Tim. 4:3-4).

Washiriki wa KANISA toka mwanzo wa vuguvugu la urejesho (urejesho wa Ukristo wa Agano Jipya) wameshindana vyema kwamba mahali au pale Mungu ametoa agizo na kutoa maelekezo iwe kwa kuagiza au kwa mfano kama kutenda agizo lililosemwa, sisi kama Wakristo, lazima tufuate agizo hilo sawasawa na lilivyoamuriwa; kama ametoa amri na kuagiza kwa

sehemu kama kwa utendaji, lazima tufuate maagizo yake kama yaendavyo na kufanya yote kadiri tuwezavyo; tena, kama Mungu ametoa amri na hatatoa maagizo ya kiutendaji, tuna uhuru wa kuata amri kwaa njia yo yote tunaweza kuonekana sahihi.

Yesu Kristo, usiku ule aliosalitiwa na maraa kufuati kushiriki Sikukuu ya Pasaka na mitume wake (Mat. 26:21-29; Mark 14:18-25; Luka 22:14-20) alianzisha kinachojulikana katika Agano Jipya kama "Meza ya Bwana" (1 Kor. 11:20, alafu pia kama "ushirika" wa mwili na damu ya Bwana (1 Kor. 10:16). Kwa wakati huo Yesu akawaagiza mitume wake "*fanyeni hivi*" (Luka 22:19). Hili ni agizo la kufanya kama alivyofanya; na kwamba ilipaswa ifanyike "*kwa ukumbusho*" wake na kifo chake (1 Kor. 11:25-26).

Pia ameagiza kwamba sehemu hii ya ibada yetu ifanyike ssiku ya kwanza ya juma (Mdo. 20:7). Siku ya kwanza ya juma inakuwa kila siku saba; hivyo Wakristo wanapaswa kushiriki kila siku ya kwanza ya juma.

Marko anasema Yesu alitwaa mkate na baada ya kuubariki aliumega na kuwapa na kusema, "*Twaeni mle; huu ndio mwili wangu*" (Marko 14:22). Neno la Kiyunani hapa lina tafsiri "*mkate*" linaweza kutafsiriwa "kipaned cha mkate" na inaelezwa hivyo kwenye maelezo ya pembeni. Mtume Paulo anaeleza, "*Sote tunakula mkate mmoja*" (au "mkate"; 1 Kor. 10:17. Pia kifungu kama hicho, "*mkate mmoja, mwili mmoja*". Kimsingi hii inazuia matumizi ya mkate zaidi ya mmoja. Ndugu wengi wanajali kidogo agizo hili mara nyingi bila kujali, lakini wengine wanafanya kusudi. Hataivyo, Wakristo wengi watakuwa tayari kukubali kwamba kunapaswa kuwepo na mkate mmoja tu. Wengi, hataivyo, wanasisitiza kwamba tunapaswa kutumia "kikombe kimoja" kwenye Meza ya Bwana.

Kulikuwa na msemo uliotumiwa na wahubiri wa zamani wa vuguvugu wa urejesho, "Inaponena Biblia, tunanena; iliponyamazaa Biblia tunanyamaza". Mwingine ameiweka hivi "Alichokifunua Mungu tunafundisha kwa furaha; ambacho Mungu hajafunua hatujaribu kukifundisha." Kadiri Wakristo wanavyoendaana na mfumo huu yote yalikuwa sawa, lakini ni ndefu, wanadamu –wanadamu tu – wakaanza kutafuta alama dhaifu (?) katika mpango wa Mungu, hivyo wakaanza kuunda-unda mpango wa wokovu kama ilivyofunuliwa na Mungu wa Mbinguni; hivyo vitu vingi vinaongozwa ili kuendana na mawazo ya wanadamu. KWA AIBU!

Mara nne katika uuanzishaji wa Meza ya Bwana imeandikwa katika Agano Jipya (Mat. 26:26-28; Marko 14:22-24; Luka 22:19-20; 1 Kor. 11:23-29) na karibia mara mbili imesemwa kwenye (1 Kor. 10:16-21). Katika vifungu hivi, "*kikombe*" (idadi ya umoja). Imetumika mara kumi na moja, lakini "vikombe" (idadi ya wingi) haijawahi kutumika kamwe katika Biblia kwa maana ya Meza ya Bwana. Kwa nini Mungu alirudia mara nyingi "*kikombe*"? Kwa nini msisitizo upo kwenye kikombe kimoja? Inawezekana ikawa hivyo, akitazama chini mika 1900 akaona kwamba wanadamu walikuwa wanaifanyia kusudi kuharibu sehemu hii takatifu ya ibada ya Wakristo? Hapana shaka juu ya hilo. Yohana anatuambia kwamba Mungu "*anafahamu mambo yote*." (1 Yoh. 3:20).

Mungu ametuonyaa mara na mara tena kuyakataa mafundisho na maagizo ya wanadamu. Tunaambiwa "*Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema;*" (1 Thes. 5:21). "*Mkihakiki ni nini impendezayo Bwana.*" (Efe. 5:10). "*Wapenzi msiamini kila roho, baali zijaaribuni hizo roho kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea duniani.*" (1 Yoh. 4:1).

Tunapaswa kuhakiki kwa kitu gani yale tunayofundishwa? Yesu anasema, "*Yachunguzeni maandiko.*" (Yoh. 5:39). Mwanahistori aliyevuviwa anatuambia kwamba watu wa Beroya walikuwa waungwana kwa sababu waliyachunguza maandiko kila siku kuona kwamba mambo waliyo hubiriwa na Paulo ndivyo yalivyokuwa (Mdo.17:11). Leo baadhi ya wahubiri wanaona kwamba ni dhambi kuhoji kile anachosema mhubiri au (nabii). Lakini Mungu aanatuambia kuwa hao wanaochunguza neno lake ni waungwana kabla hawajaukubali, hata kama mwalimu ni mtume wetu.

Wakati fulani Yesu aliwauliza baadhi ya Wayahudi, "*Ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni au kwa wanadamu? Mnijibu!*" (Marko 11:30). Ninawauliza watu wa, "Elimu ya vikombe vingi; je imetoka mbinguni au kwa wanadamu? Mnijibu!" watu hawa wanafahamu imetoka wapi, wanafahamu ni kwa wanadamu. Yesu tena akasema, "*Enyi wanafiki ni vyema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu akisema, watu hawa uniheshimu kwa midomo; ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*" (Mat. 15:7-9). Alfu akaongeza (Ms 13) "*kila pando alilolipanda baba yangu wa mbinguni halitang'olewa*." Na ms 14, "*Waacheni hao ni viongozi vipofu…*" Paulo alimwambia Tito (Tito 1:13-14) "*Ushuhuda huo ni wa kweli. Kwa sababu hiyo uwakemee kwa ukali, ili wapate kuwa wazima katika imani; wasisikilize hadithi za Kiyahudi, wala maagizo ya watu wajiepushao na yaliyo kweli.*"

Musa akimnukuu Mungu kuhusiana na kuja kwa Kristo, "*BWANA akaniambia wametenda vyema kusema walivyosema. Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. Hata itakuwa mtu asiyesikilizaa maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake. Lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au aatakayenena kwa jina la miungu mingine, nabii yule atakufa.*" (Kum. 18:17-20).

Mtume Paulo alisema kwamba kwa uvuvio wa maandiko mtu wa Mungu amekamilika, "*Amekamilishwa katika matendo mema*" (2 Tim. 3:16-17). Neneo la Mungu haliwakamilishi "vikombe vingi", kwa sababu, "vikombe vingi" haiwezi kuwa kazzi njema; na kama siyo kazi njema, lazima iwe kazi ovu. Ni wazi kwamba hawa watu wa vikombe vingi hawamwamini Paulo, na kwa vile Paulo aliandika ufunuo wa Yesu Kristo (Gal. 1:11-12) hawamwamini Kristo.

Tunasoma katika 2 Pet.1:3, "*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa.*" Yesu Kristo alituita; tunao ujuzi wake tuliopewa katika Agano Jipya. Vyote vipasavyo uzima (uzima wa kiroho) na Uungu vinapatikana katika Agano Jipya,

watu wa vikombe vingi kwa vile haipatikani pale hawana “uzima na Uungu”; wanapaswa kufa (kifo cha kiroho) na ushetani. Kutoridhika, chuki, kuvutana, ugomvi, wivu, na mgawanyiko vyote vinavyotokana na matumizi yao unadhihirisha, kama uthibitisho utahitajika, kwamba vinapaswa kifo na ushetani. Mara nyingi Shetani anapiga palipo na mpango mzuri ili kugawanya majeshi ya Kristo, angamiza nafsi za watu na kuwaleta motoni kwake anapowapatia “vikombe vingi”. Sulemani alisema, “*Tazama hili tu nimeliona; Mungu amemfanya mwanadamu mnyofu, lakini wamebuni mavumbuzi mengi.*” (Mhu. 7:29).

Kusanyiko lolote linalotumia “vikombe vingi” imeyapita mafundisho ya Kristo. “*Basi ndugu zangu mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa; ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe.*” (1 Kor. 4:6). “*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.*” (2 Yoh.1:9). Kuwa bila Mungu ni kuwa bila tumaini (Efe. 2:12).

“*Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; naye akisita-sita roho yangu furaha naye.*” (Heb. 10:38). “*Imani huja kwa kusikia neno la Mungu.*” (Rum. 10:17). Hakuna neno la Mungu kwa kile tunachofanya – hakuna imani. “*Na kila tendo lisilotoka kwa imani ni dhambi.*” (Rum. 14:23). “*Pasipo imani haiwezekani kumpendeza.*” (Heb. 11:6). Lakini wengine wanaweza kuuliza, “Thambi ni nini?’ Mungu anajibu, “Thambi ni uasi” (1 Yoh. 3:4). Uasi ni nini? Ni hali ya kuwa bila sheria. Sheria ya “vikombe vingi” iko wapi?”

w. G. Roberts, muhubiri anayefahamika vizuri na mmoja wa wafanya midahalo miongoni mwa makanisa ya Kristo miaka kadhaa alisema hivi, “Uanzishwaji wa matumizi ya vikombe vingi unasababisha mgawanyiko na machukizo (Rum. 16:17-18) ambayo ni kosa. Ni chukizo ambalo haliwezi kuwekwa kwenye mtazamo wa udhaifu, usiseme kitu kuhusu ndugu wenye nguvu wanaokataa.”

Wote wanakubali kwamba kikombe kimoja ndiyo njia salama; kwa nini tusafiri kwenye njia tusiyokuwa na uhakika nayo? Barabara yenye maswali, barabara isiyotufikisha kwenye milango ya mji wa Mungu mji war aha, sehemu ambayo hakuna huzuni, hakuna kukatishwa tamaa, hakuna machozi, sehemu ambayo Yesu alikwenda kutuandalia. (Ufu. 21:1-7; Yoh. 14:1-3).

Tunafahamu kwamba njia ya vikombe vingi inamashaka tena ni njia ya mgawanyiko na katika kuifuata inamanisha kwamba hatujali ombi la Bwana wetu ya umoja wa Wakristo (Yoh. 17:11) haijawahi kujibiwa, hakika inamanisha kwamba tunarusha kutabu hicho cha maombi usoni kwa Yesu. Mgawanyiko unasababishwa na baadhi ya watu wanapoondoka kutoka katika neno la Mungu. Ndugu wanapoendelea kufanya kitu katika kazi na ibada ya kanisa ambayo haiwezi kuungwa na maandiko ya Agano Jipya mgawanyiko ni lazima. Hivyo wale wanaohusika na kuanzisha au wanaendelea na mafundisho hayo ambayo hayapo au kuyafanya wanahatia ya jumla kutotii agizo la Bwana. “*Basi ndugu nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka bali mhitimu katika nia moja na*

shauri moja." (1 Kor. 1:10). "*Ndugu zangu nawasihi waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo; bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini nay a kujipendekeza wataidanganya mioyo ya watu wanyofu.*" (Rum. 16:17-18). "*Kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana ikiwa kwenu kuna husuda na fitina je! Je si watu wa tabia ya mwilini ninyi, tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?*" (1 Kor. 3:3). Moja ya vitu saba anavyovichukiaa Yehova ni "*Naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu.*" (Mit. 6:16-19).

"*Na nyumba ikifitinika juu ya nafsi yake, nyumba hiyo haiwezi kusimama.*" Marko 3:25.

"*Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa mwitu wakali wataingia kwenu wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.*" (Mdo. 20:29-30).

Mbwa mwitu wapo miongoni mwetu, hawaliachi kundi, "*nyumba ya Mungu"* (1 Tim. 3:15) inagawanyika yenyewe. Ni wakati gani itasimama.

Hawa watu wa vikombe vigi hawaridhiki na njia ya Kristo ya kufanya mambo na kwa matendo yao, yanayoongea kwaa sauti kuliko maneno yao, wanasema, "Hatujali kile anachosema Mungu, tunakwenda kupanga kazi na ibada ya kanisa jinsi tunavyodhani na sahihi."; kana kwamba ni werevu kuliko Mungu. Sawa, kimsingi wanasema, "tunamwanga saivi zaidi" (kuliko Agano Jipya lilipoandikwa). Kweli, mwanadamu amejifunza mengi karibia miaka 2000 iliyopita, lakini Mungu hajajifunza kitu kipya, kwa sababu rahisi kwamba kila kitu kilikuwa kipya mwanzo; "*Na kwa sababu hakuwa na haja ya mtu kushuhudia habari za wanadamu; kwa maana yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu.*" (Yoh. 2:25). "*Ikiwa mioyo yetu inatuhukumu kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote.*" (1 Yoh. 3:20). Alitupa sheriaa kamilifu (Yak. 1:25). Badiliko lolote, kuzidisha au kutoa inaweza kuifanya isiwe kamilifu na kuleta hukumu juu ya mtu yeyote au kundi la watu walio na hatia ya tendo hilo; "*Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya nmna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwaa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na <u>alaaniwe</u>. Kama tulivyotangulia kusemaa, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea na <u>alaaniwe</u>. Maana sasa je ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendezaa wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.*" (Gal. 1:6-10). Watu wa vikombe vingi wanauhakika wa kutafta kuwapendeza wanadamu. Na wanauhakika kwamba siyo watumishi wa Kristo.

Tupende au tusipende, tunakwenda kuhukumiwa siku ya mwisho kwa injili ya Yesu Kristo, neno lililoandikwa la Agano Jipya. Yesu alisema (Yoh. 12:48), "*Yeye anikataaye mimi asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu*

siku ya mwisho." (Rum. 2:16) "*Katika siku zile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na injili yangu, kwa Kristo Yesu.*" (Yak 2:12) "*Sheria kamilifu*" (Yak. 1:25).

Ninaweza kusema, "Mimi ni mkweli na mwaminifu, ninafanya kile ninachodhani ni sahihi; ninadhani kama nikimwabudu Mungu katika roho wa kweli, hilo ndio jambo la msingi." Hii ni elimu ya kawaida miongoni mwa Wakristo wanaokiri leo kila mahali, hata miongoni mwa ndugu wa makanisa ya Kristo. "*Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu wa uongo wengi wametokea duniani.*" (1 Yoh. 4:1). Ndiyo, "*kwa maneno yao laini na matamu*" wanawadanganya watu wengi wema. Mungu atawajali manabii wa uongo, lakini vipi kuhusu mimi kama nikidanganywa? Hakika Mungu hatanihukumu; au atanihukumu? Ebu tuone. "*Kipofu akimuongoza kipofu mwenzake wote wawili watatumbukia shimoni.*" (Mat. 15:14). "*Wakapanda juu ya upana wan chi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa. Moto ukashuka kutoka mbinguni ukawala. Na yule ibilisi mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele.*" (Ufu. 20:9-10). Wale "*wanaodanganywa*" ndiyo "*siyo wakweli,*" wa kweli na waaminifu wanaofanya kile wanachofikiria ni sahihi, kuabudu "*kwa roho wa kweli*", lakini "*walidanganywa*" na shetani akifanya kazi kupitia manabii wa uongo (wahubiri na waalimu) na "*Moto ukashuka kutoka mbinguni ukawala.*"

Tunasoma katika Warumi 15:4, "*Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na matumaini.*" (Soma pia 1 Kor. 10:11). Hebu tujifunze somo kutoka katika mfano sura ya kumi na tatu ya 1 Wafalme. Mtu waa Mungu (nabii) kutoka Yuda alikuwa mtu mzuri, mtu mwaminifu, na mkweli; alibeba uhai wake mkononi ili kufanya kazi ambayo Mungu alimpa. Lakini nabii mwingine alipomwambia uongo, aliamini na kutii uongo huo na matokeo yake akapoteza uhai wake. Alikuwa ni mmoja wa kweli aliopokelewa. Paulo alisema, "*Na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili waahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu.*" (2 Thes. 2:10-12).

Katika 1 Kor. 10:21 and 11:27, mtume katika kuongelea Meza ya Bwana akiongelea "*Kikombe cha Bwana.*" Wanaume wawili wa Kristo walikuwa wanaongelea Meza ya Bwana; Ndug. T. akasema, "Angalia tangazo hilo hapo, ukiikata na kuigawanya tangazo lako litakuwa wapi?" hakutakuwa na tangazo. Na kama ukigawanya kikombe cha Bwana katika idadi ya vikombe kikombe cha Bwana kiko wapi?

Baadhi ya udhuru wa kawaida

"Kombe cha kawaida siyo kisafi."

Jibu:

Huu ni udhuru tu, siyo sababu ya Biblia, kwa kutumia vikombe vingi katika ushirika. Nimefahamu matukio mengi ya sinia lililojaa vikombe vikipitishwa kwa watu 15 au 20 ambao wamekunywa mvinyo na hakukuwa na kikombe kilichobaki tupu. Alafu hakuna pingamizi lililofanywa. Mkate wa kawaidaa unatumika. Washiriki wote wanaushikilia mkate huo, alafu tunaambiwa kwamba wadudu wanakuwepo karibia mara kumi mikononi na kwenye kinywa. Kusanyiko la Wakristo ni hadhira safi ulimwenguni, wasafi kama nguo na yenye afya kama miili na matumizi ya kikombe cha ushirika chini ya mazingira hayo inasisitiza ubora wa usafi wa Mkristo, wakati matumizi ya vikombe vingi inapingana na mafanikio ya Mkristo na inaleta uoga katika upande wa kila mshiriki kuhusiana na wengine na zaidi inakosa umuhimu wa uboreshaji. Hakika ningeweza kuwa na imani ndogo katika Bwana Yesu Kristo ikiwa ningeamini kwamba angeniagiza kufanya jambo ambalo lingedhuru afya yangu. Kwa zaidi ya miaka 1900 Wakristo walikutana kuabudu na kuula mkate mmoja na kukinywea kikombe kimoja na kupitia karne zote hizo vikombe vingi havikusikika. "*Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona*." (Mat. 16:25).

Nimekuwa nikijiuliza kama kumekuwa na mtu aliyedhurika kwa matumizi ya kikombe kimoja katika Meza ya Bwana.

Ndugu J. W. McGarvey mmoja wa wanafunzi wa kubwa wa Biblia toka siku za mitume na maranyingi alinukuu kama mamlaka leo, wakaati fulani aaliulizwa, "Nimekuwa mshiriki wa kanisa la Kristo kwa miaka 43 na imekuwa ni bahati kwangu na nimekuwa nikifahamika sana na wasomi na wahudumu wenye mvuto, A. Campbell miongoni mwao, na inaonekana kitu kigeni kwangu kwamba hawakuona umuhimu wa kuwepo "vikombe vingi."

Ndugu McGarvey akajibu, "Siyo kitu kigeni kabisa; maana umuhimu kama huo haujagundulika. Kutamani jambo hili kumetokana na ugonjwa walioupata baadhi ya wanawake, na inaungwa mkono na daaktari mpya miongoni mwa madaktari kuhusu vijidudu, wadudu wadogowadogo wanaoning'inia vinywani mwa watu, wanakaa kwenye kikombe, alafu uhamia kwenye kinywa cha mtumiaji anayefuata, alafu wanashuka tumboni kwa mtumiaji, Wanakaa katika kiungo chake cha muhimu, na kula vinavyokutwa pale hadi magonjwa ya ajabu yaibuke. Sifahamu ni watu wangapi wamefariki kutokana na ugonjwa huu toka bwana alipoanzisha huduma hii, lakini nadhani alifahamu ni nini kingekuwa madhara naa akabeba majukumu. Kama daktari wetu ye yote amewahi kutibu tatizo kama hili kama inavyotakiwa, sijawahi kuwasikia; na ninapenda kuweka ahadi yangu hatarini, masikini kama niishivyo, wafu wote watakaokufa kutokana na sababu hii. Wote watakufa kwa wakati wao, na watahitaji mazishi mazuri.

Akaendelea kueleza: "Udhuru unaotolewa mara nyingi ni 'kuacha kueneza ugonjwa'. Sawa na sababu nzuri kwamba tunapaswa kuwa na nguo ndefu ya ubatizo itakayomzuia mbatizwaji asilowe, ili kumsaidia asipate baridi, kama wengine 'wanavyodhani' kwamba ni hatari kubatizwa wakati wa hali ya baridi. Au tunaweza 'kudhania' kwamba ubatizo uachwe hadi hapo hali ya joto itakapokuja katika misingi hiyo 'wanayodhani' kuwa tunapaswa kuwa na vikombe vingi. Kikombe kimoja hakiambukizi ugonjwa sasa kuliko ilivyokuwa miaka 100 iliyopita. Lakini

Bwana hakuanzisha kisaambaza ugonjwa alipoanzisha Meza ya Bwana. hayupo mtu hata mmoja ambaye amewahi kupata ugonjwa kwa kubatizwa kwenye maji yenye mazingira ya baridi, au yeyote kupata ugonjwa kwa kunywa katika kikombe ambacho wengine wamekinywea. Hicho ni kitu kilichoanzishwa na Bwana, na atawajali mwanaume au mwanamke wa imani.

Kwa vile imegindulika kwamba wadudu wenye ugonjwa wanaingia mwilini kupitia hewa tunayopumua na chakula tunachokula. Hiyo kuwa kweli kuna kinga kiasi gani uliopo "washiriki wa vikombe vingi? Kila mmoja anaweza kuona kwamba madahalo wa "afya" ni muhimu.

Sheria inazuia matumizi ya kikombe kimoja.

Jibu:

Kuna sheria Marekani inayozuia matumizi ya kikombe kimoja katika ibada ya Kikristo. Marekebisho I ya katiba yetu inasomeka, "Bunge halitatunga sheria inayotii au inayoanzisha dini au inayozuia maendeleo ya uhuru." Na kila jimbo limepewa mwongozo huo kwenye katika yao.

"Kusanyiko kubwa haliwezi kuhudumiwa kwa kutumia kikombe kimoja pekee."

Jibu:

Kusanyiko likiwa kubwa kuweza kutumia kikombe kimoja, ni kubwa kutokana na maendeleo ya washirika wake. Mhubiri maarufu na muhariri aliandika miaka kadhaa iliyopita: "Hivi karibuni alipokuwa akiwasiliana na mzee wa kanisa kubwa ambalo lina washiriki mia, niliondoa sifa ya idadi kubwa ya wanaume ambayo ilitengenezwa pale, lakini alinipa uelewa kwamba kulikuwa na wanaume wachache pale walio na uwezo wa kulifundisha kanisa kwa njia ya kulielimisha." Yawezekana msingi huu ukazalisha sababu kadhaa.

- Inaudhi sana mtu anapotoa kauli ya kwanza mbele ya wasikilizaji wengi. Hawezi kulifanya.
- Zamu ya mtu kunena haitakuja mara nyingi vya kutosha, ili kumfanya ajiandae.
- Kusanyiko kubwa karibia wakati wote linapata "mchungaji" mhubiri, alafu wanakaa na kumsikiliza kila siku ya Bwana na kwenye kila mkutano.
- Washirika wa kusanyiko kubwa hawafahamiani, palipo na kutofahamiana kuna ukosefu wa uruma, palipo na ukosefu wa huruma kuna ukosefu wa ushirikiano na msaada wa ukarimu ambayo ni muhimu katika maisha ya Ukristo.

Wanatuambia kwamba kanisa la Yerusalemu lilikuwa kubwa. Ndiyo, kwa wakati mmoja kanisa la Yerusalemu lilikuwa na washiriki karibia 10,000, lakini hakuna ushaidi unaoonyesha kwamba wote walikusanyika sehemu moja. Hakukua na nyumba kwenye mji huo ambayo ingeweza kuwabeba watu hao. Hataivyo, tunao ushahidi kwamba kanisa la Yerusalemu pamoja na nyingine walikutana makundi machache katika sehemu tofauti ya mji huo. Katika Mdo.12:12 baada ya malaika kumwachia Petro kuwa huru kutoka gerezani na kuondoka, tunasoma "*Na*

alipokuwa akifikiri haya akafika nyumbani kwa Mariamu, mamaye Yohana ambaye jina lake la pili ni Marko; na watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba." Na kwenye msitari wa 17 tunasoma tena, "*Naye* (Petro) *akawapungia mkono wanyamaze, akawaeleza jinsi Bwana alivyomtoa katika gereza. Akasema kampasheni Yakobo na wale ndugu habari hizi. Akaondoka akaenda mahali pengine.*" Hivyo, kulikuwa na ndugu waliokutana sehemu zingine. Kwamba kanisa la kwanza lilikutana katika makundi madogo inaonyeshwa zaidi kutokana na ukweli kwamba kulikuwa na makusanyiko matatu katika Rumi (Rum. 16:5, 14-15). Angalia pia Kol. 4:15; 1 Kor. 16:19; Filemoni 2; Rum.16:1. Vifungu hivi pia vinaonyesha sehemu ya kanisa la Korintho likikutana Kenkrea, kitongoji.

Kusanyiko kubwa linalojisimami haliwezi kumaliza idadi ya wema miongoni mwa watu wa dunia kwamba makusanyiko kadhaa machache yametawanyika miongoni mwa jamii inavyoweza kufanya.

"Luka 22:17 inatoa mamlaka ya matumizi ya vikombe vingi: 'Naye akakipokea kikombe na baada ya kushukuru akasema twaeni mgawane."

Jibu:

Kifungu hiki hakina uhusiano na wala hakiongelei meza ya Bwana, lakini kilikuwa ni kinywaji kilichotolewa kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka (angalia Hesabu 15:1-5) ambayo mara ikapelekea uanzishwaji wa Meza ya Bwana. [kinywaji katika Luka 22:17 ilikuwa ni sehemu ya sherehe ya Pasaka; hataivyo, ilikuwa haihusiani na kinywaji kilichotolewa ya Hesabu 15:1-5 – Ellis Forsman]

Katika 1 Kor. 10:16 Paulo anasema, "*Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo.*"

"Yesu aliposema '*Kikombe*' alimanisha uzao wa mzabibu."

Jibu:

Sasa tunapaswa kuamini kwamba Yesu Kristo alikuwa mkaidi kwamba hakujua namna ya kujieleza, au hakufahamu alichokuwa anakiongea?

Lakini Biblia inatuambia "*Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhalimu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu.*" (1 Kor. 1:25 na "*Maana hekima ya dunia hii ni upuzi mbele za Mungu.*" Kama Bwana angesema ameibariki uzao wa mzabibu tungekuwa na haki ya kutumia vikombe vingi tutakavyo, lakini kuwa na kanuni ya umoja wa mwili alitumia neno "*kikombe*". "*Wote wakakinywea.*" ("*kikombe*") (Marko 14:23). Tena, tunasoma katika 1 Kor. 11:23-28 kwamba Yesu "*alitwaa kikombe.*" Matamshi halisi (yaitwayo yenyemaana sawa) ambayo sehemu inawekwa kwa ajili ya yote (kama "safari hamsini" kwa meli hamsini). Katika swala hili kikombe kinawekwa kwa ajili ya kikombe na faharisi. Kwamba Bwana akakibariki kikombe pamoja na faharisi yake inathibitishwa kwa neno ya Kiyunani

“poterion” ikitafsiriwa “*Kikombe*” katika Mathayo 26:27; Marko 14:23 na kwingineko. Kamusi ya Lexicographer of The Literary Dugest inasema “neno ‘*kikombe*’inatumika kiuhalisia.” Kwa hili inakubali Wanafunzi wa Kiyunani walioko Marekani (James H. Ropes, wa Chuo cha Harvard Edgar J. Goodspeed, wa Chuo cha Chicago; Harry M. Hubbel, wa Chuo cha Yale; C. A. Savage, wa Chuo cha Minnesota; W. C. McCown, wa Chuo cha California; R. A. Jernberg, wa Chuo cha Southern California; E. E. Stringfellow, wa Chuo cha Drake, Des Moines, Iowa; na wengine wengi.).

Maelfu ya maneno – kurasa juu ya kurasa – vimeandikwa, hotuba juu ya hotuba imehubiriwa, katika jitihada za kuonyesha kwamba vikombe vingi katika ushirika wa meza ya Bwana ni bora kuliko kikombe kimoja. Kazi yote hii na gharama ingeweza kutumika katika kuandaa kifungu kimoja toka katika andiko takatifu; lakini humo kuna uongo katika ugumu wao; hawajaweza kupata andiko hilo dogo.

“*Na tena Bwana anafahamu mawazo ya wenye hekima ya kwamba ni batili.*” (1 Kor. 3:20).

Sasa rafiki yangu, nitakwambia sababu ya hamu kubwa ya “vikombe vingi”. Mmoja akasema, “ni kawaida; ni ya kisasa na maarufu.” Kiburi, au hamu ya kutaka kuwa “*kama mataifa yote*” (1 Sam. 8:2) ndiyo kinachoita “vikombe vingi;” na kiburi ni dhambi. Mvuto, au mtazamo wa kitu, ndicho kinacho chukua macho ya hao wanaotaka vitumiwe. Kiburi ni “mwanaume” iliyowatambulisha na kama tukikubaliana na “mwanaume” katika hili tutapaswa kutoa katika tukio fulani wakati ambapo hatutapenda kufanya hivyo.

Yesu alisema, “*Ole wenu ninyi watu wote watakapowasifu, kwa kuwa baba zao waliwatendea manabii wa uongo mambo kama hayo*.” (Luka 6:26).

Katika sura ya pili ya Kol. na msitari wa nane tunasoma, “*Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo.*” Tunapokutana pamoja katika meza ya Bwana inaonekana kwamba mwana ye yote wa Mungu atatamani kufanya kitu kilekile alichoagiza Kristo. Fikra yake ya juu inapaswa kuwa, “Bwana, unataka tufanye nini?” Agizo chanya linahitaji utendaji, kwa njia fulani, kwa tendo halisi, siyo muhimu zifanane, kwa ajili ya mwisho mzuri. Sifa haipo katika tendo pekee bali katika utii wa mamlaka. Zinapoungana na matendo halisi matendo haya ni ya muhimu katika utii wa maagizo. Matendo haya yanafanya kazi kwanjia fulani ya agizo; hivyo hakuna utii pasipokuwa na tendo au matendo yaliyoagizwa. Maagizo chanya inahitaji roho dhabiti wa utii kwa maagizo ya Mungu kupitia Kristo katika kanisa lake na kuheshimu mamlaka yake katika nyumba yake na meza yake.

“*Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani, msishike, msionje, msiguse; mambo hayo yote uharibika wakati wa kutumiwa; hali mkifuata maagizo na mafundisho ya wanadamu? Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika namna ya ibada mliojitungia*

wenyewe na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzizuia tamaa za mwili." (Kol. 2:20-23).

Kama ungeandaa sherehe na ukawakaribisha wageni kadhaa, ambao wakiwa wanawasili, hawakupenda jinsi chakula kilivyopangwa, wakafika na kuanza kupangua, je ungependa jambo hilo? Hapana! Unaweza kudhani wageni hao wanakusudi; usingependa tabia zao. Bwana hapendi wageni wake kupangua kwa makusudi meza yake au kitu kingine chochote katika nyumba yake, kanisa (Kum. 18:20).

Kama ukiniajiri, na nikawa naafanya vitu ambavyo hukuniagiza au kufanya vitu tofauti na ambavyo unataka, ninauhakika utanifukuza. Ninahofia kwamba wengi wanaojiita wakristo wanakwenda kumsikia Bwana wa mbinguni na dunia akisema "*Ondokeni kwangu.*" (Mat. 25:41).

Tuangalie somo lingine kutoka Agano Jipya. Katika Law10:1-2 tunaambiwa kwamba manabii wawili (Nadabu na Abihu) waliangamizwa na moto mbele ya Yehova, siyo kwamba walishindwa kufanya kitu ambacho Mungu aliwaagiza bali kwa sababu walifanya kitu ambacho Mungu <u>hakuwaagiza.</u> Hiki ndicho watu wa vikombe vingi hufanya.

Mwanzo wa harakati za urejeshi kanisa liliungana bila kuwepo kwa vikombe vingi. Leo kanisa limegawanyika, na ni kwa sababu ya vikombe vingi. Wale walioanzisha "vikombe vingi" hakika wanahusika na mgawanyiko huu.

Wafuasi wote wa Kristo wanaokiri wanakubaliana kwa yafuatayo:

- Jina "*Wakristo*" (Mdo. 11:26; 1 Pet. 4:16).
- Wanapaswa kukusanyika wenyewe (Heb. 10:25).
- Lazima wakutane kila siku ya kwanza ya juma (Mdo. 20:7).
- Kwamba ni haki kushiriki meza ya Bwana na kuwa na mahubiri siku ya kwanza ya juma (Mdo. 20:7).
- Matumizi ya kikombe kimoja katika meza ya Bwana ipo kimaandiko na salama (Mk. 14:22-24)
- Ubatizo ni haki (Mat. 28:19).
- Ubatizo wa kuzikwa majini ni salama (Rum. 6:4).
- Kutoa fedha zetu (1 Kor. 16:2).
- Kuomba (Mdo. 12:5).
- Kuimba nyimbo za kimaandiko (Kol. 3:16).
- Kusoma, kuhimiza na kufundisha Biblia (1 Tim. 4:13)
- Kusaidia wenye mahitaji na kuishi maisha masafi (Yak. 1:27).
- Kufanya kazi ya umisioni (Marko 16:15; Fil. 4:15-16).
- Kanisa linapaswa kuwa na wazee, mashemasi, na wainjilist (1 Tim. 3; 2 Tim. 4:5).

Ndio, wote wanakubali kwamba vitu hivi ni sahihi na salama, na kwamba tukivifuata kwa uaminifu tutaufikia mji huo ambao Yesu amekwenda kuwaandalia watu wake (Yoh. 14:1-3). Ni pale tunapoanza kufanya vitu ambavyo havipo kwenye injili, mafundisho na maagizo ya wanadamu ndio chanzo cha mgawanyiko.

"*Tazama kutii ni bora kuliko sadaka za kuteketeza, na kusikia kuliko kondoo wenye mafuta.*" (1 Sam. 15:22)

Wapo ndugu wengi wanaopenda kikombe kimoja, ambao wanamashaka ya kimaandiko na usalama wakitumia vikombe vingi, lakini "nenda pamoja" kuliko kuleta usumbufu kwenye kusanyiko. Ninamfahamu mtu ambaye kwa miaka mingi, alikunywa uzao wa mzabibu kwa kutumia vikombe vingi na alipofanya hivyo moyo wake ulimsuta. "*Ikiwa mioyo yetu inatuhukumu; kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote.*" (1 Yoh. 3:20). Ndiyo, atatuhukumu. "*Najua tena nimehakikishiwa katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake*." (Rum. 14:14). Na katika msitari wa 23, "*Lakini asiye na shaka kama akila amehukumiwa kuwa na hatia, kwa maana hakula kwa imani. Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi.*"

Je una mashaka?

Mtu Petro anatuambia (2 Pet. 1:10), "*Kwa hiyo ndugu jitahidini sana kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu.*"

Kama tukifanya ambacho injili inatuambia kufanya na ambacho wakristo wote wanaokiri wanakubali kuwa ni sahihi na salama, hatutahukumiwa; hakika tutafanya wito wetu na uteule wetu imara.

Ndugu, afadhali uwe imara!

Watu wengi wanakubali wenyewe baada ya dhamira zao "kuchomwa na pasi," kama mlevi angeweza kujisifu baada ya muda, hata kama mara ya kwanza alihisi anahatia ya kunywa kikombe kimoja cha pombe. Mwishowe ni ulevi. Mwisho wetu utakuwa nini kama tukiendelea katika njia ya mashaka? Ninaogopa itakuwa kama katika Mat. 7:21-23.

"*Basi ndugu simameni imara mkayashike mapokeo mliofundishwa, ama kwa maneno ama kwa waraka wetu.*" (2 Thes. 2:15)

Tafadhali soma tena maombi hayo makuu ya Bwana katika Yohana 17:11.

Kwa maombi ya kila mara na matumaini kwamba wale wanaosoma kipeperushi hiki watashindania kutunza umoja wa Roho katika kifungo cha imani.

Mimi ni ndugu yenu, F. H. Stringham